TANGAZO LA SERIKALI NA. 197 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,

SURA YA 415

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 61(1) na (2)(a) na (b))

KANUNI ZA UGOMBOAJI NA UONDOSHAJI WA BIDHAA ZA KIPEKEE ZA MWAKA 2025

MPANGILIO WA KANUNI

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

kanuni *jina*

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UTOAJI WA HUDUMA ZA KIPEKEE ZA UGOMBOAJI NA UONDOSHAJI

4. Huduma za kipekee za ugomboaji na uondoshaji.
5. Huduma zitakazotolewa na Shirika.
6. Kutekeleza kazi ya wakala binafsi wa meli.

SEHEMU YA TATU
MAKUBALIANO NA MTU WA TATU

7. Kutekeleza majukumu ya Shirika.
8. Kushirikishwa kwa mtu wa tatu aliye na leseni au aliyesajiliwa.
9. Upatikanaji wa mtu wa tatu.
10. Masharti ya utoaji wa huduma.

11. Kamisheni inayolipwa kwa mtu wa tatu.
12. Uwajibikaji wa mtu wa tatu.

SEHEMU YA NNE
ADA, TOZO NA KAMISHENI

13. Ada, tozo na kamisheni zinazotumika.
14. Akaunti ya amana ya mteja.
15. Matumizi ya bakaa ya fedha ya mteja.
16. Njia na masharti ya malipo.
17. Kushindwa kufanya malipo.
18. Malipo ya kamisheni.
19. Malipo ya sehemu ya utendaji.

SEHEMU YA TANO
VIGEZO NA MASHARTI YA BIASHARA

20. Utaratibu wa bima.
21. Maelekezo ya mteja.
22. Uwasilishwaji wa shehena.
23. Upokeaji wa shehena.
24. Dhamana ya shehena.
25. Uthibitisho wa taarifa sahihi.
26. Fidia.
27. Wastani wa jumla.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA JUMLA

28. Ukomo wa madai ya hasara au uharibifu.
29. Wajibu wa Shirika.
30. Tathmini ya fidia.
31. Ukomo wa fidia.
32. Ukomo wa uwajibikaji kwa kuchelewaji.
33. Jukumu la usiri.
34. Uzingatiaji wa taratibu zilizoanzishwa za biashara.
35. Utaratibu wa kushughulikia malalamiko.
36. Kufuta.

SHERIA YA UWAKALA WA MELI TANZANIA,

SURA YA 415

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 61(1) na (2)(a) na (b))

KANUNI ZA UGOMBOAJI NA UONDOSHAJI WA BIDHAA ZA KIPEKEE ZA MWAKA 2025

SEHEMU YA KWANZA MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Ugomboaji na Uondoshaji wa Bidhaa za Kipekee za Mwaka 2025.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwa Shirika, mteja au mtu wa tatu wakati wa kutekeleza au kupokea huduma za ugomboaji na uondoshaji wa bidhaa za kipekee katika kuingiza ndani ya nchi au kutoa nje ya nchi kutoka Tanzania Bara.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo:

Sura ya 415

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;

Sura ya 415

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 21 cha Sheria;

"nyaraka ya mzigo" inajumuisha hati ya usafirishaji, hati ya usafirishaji wa anga, nyaraka ya usafirishaji wa mzigo kwa njia ya barabara, manifesti, nyaraka ya shehena, ankara, nyaraka ya orodha ya usalama wa mizigo, kibali cha kuingiza ndani ya nchi au kutoa

nje ya nchi, mpango wa upangaji, mpango wa kuhifadhi, orodha ya upakiaji na orodha ya upakuaji;

Sura ya 182

"kemikali" ina maana kama ilivyoelezwa chini ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, na kwa madhumuni ya Kanuni hizi, inahusiana na:

(a) kemikali zilizoagizwa na kampuni ya uchimbaji madini; au
(b) kemikali zinazotumiwa na kampuni za uchimbaji madini,

bila kujali kama msafirishaji ni kampuni ya uchimbaji madini au siyo kampuni ya uchimbaji madini;

"Shirika" maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria;

"mteja" maana yake ni mtu ambaye anapata au anataka kupata huduma kutoka kwa Shirika na inajumuisha msimamizi mkuu wa meli, wakala wa meli, msafirishaji na mwenye mzigo;

"kuondoa mzigo kwenye kontena" maana yake ni mchakato wa kutoa mzigo kutoka katika kontena kwa ajili ya kusafirishwa au kufikishwa kama mzigo usio katika kontena;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 30 cha Sheria;

"wastani wa jumla" maana yake ni mgawanyo wa wajibu wa kifedha kwa msafirishaji, mwenye mzigo au mtu mwenye maslahi na hasara itokanayo na kutupa mzigo kwa dharula;

Sura ya 283

"nyara ya Serikali" maana yake ni nyara ya Serikali kama ilivyorejewa chini ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori;

"taratibu za ndani za uendeshaji" maana yake ni taratibu zilizoidhinishwa kwa mujibu wa kifungu cha 22(2)(d) cha Sheria ili kuliongoza Shirika katika kutekeleza majukumu yake;

"mnyama hai" maana yake ni aina yoyote ya mnyama mwenye uti wa mgongo na asiye na uti wa mgongo na mnyama mdogo na yai lake, isipokuwa wanyama wa kufugwa;

"manifesti" maana yake ni nyaraka inayotoa orodha kamili ya mizigo kwenye meli, jina la meli na inajumuisha taarifa na maelezo ya kila hati ya usafirishaji ya mizigo yote, jina la nahodha wa meli na wakala wa meli kwenye bandari husika ya kupakia au kushusha;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya usafirishaji kwa njia ya maji;

Sura ya 123 "makinikia ya madini" ina maana sawa kama ilivyoelezwa chini ya Sheria ya Madini;

"mteja wa mara moja" inahusu mwingizaji ndani ya nchi au msafirishaji nje ya nchi wa bidhaa ambaye hujihusisha na Shirika katika usafirishaji wa mzigo mara moja tu bila matarajio au nia ya kusafirisha mizigo mingine katika siku za usoni;

"namba ya udhibiti wa malipo" maana yake ni namba ya kumbukumbu inayotengenezwa kutoka Serikalini pamoja na ankara ya kodi kwa ajili ya kufanya malipo ya mtandaoni kwenye akaunti ya ukusanyaji wa mapato ya Shirika;

"viwango vya utendaji" maana yake ni viwango vya utendaji vilivyowekwa na Shirika ili kuzingatiwa na mtoa huduma;

Sura ya 166 "bandari" ina maana sawa kama ilivyoainishwa chini ya Sheria ya Bandari;

"msimamizi mkuu wa meli" maana yake ni msafirishaji wa baharini ambaye wakala wa meli hufanya kazi kwa niaba, katika biashara ya usafirshaji wa meli;

"nyaraka za wakala wa usafirishaji wa meli" maana yake ni nyaraka zinazotolewa na msafirishaji wa baharini au wakala wa msafirishaji ili kuambatishwa na ombi la kuidhinishwa na forodha au mamlaka nyingine kwa ajili ya usafirishaji kwa meli, mizigo, abiria na huduma za melini na inajumuisha hati ya usafirishaji, hati ya usafirishaji wa anga, manifesti, nyaraka ya uwasilishaji wa mzigo, hati ya usafirishaji kwa meli, au nyaraka nyingine yoyote husika katika tasnia ya usafirishaji wa majini kama inavyoweza kuainishwa na mamlaka husika;

"nyaraka ya usafirishaji" maana yake ni nyaraka sahihi ya usafiri inayowezesha ugomboaji wa shehena kupitia

forodha, bandari na mamlaka nyingine na inajumuisha hati ya usafirishaji, hati ya usafirishaji wa anga, manifesti, ankara, orodha ya kupakia, nyaraka ya uwasilishaji wa mzigo, hati ya usafirishaji wa kwa meli, hati ya bima au nyaraka nyingine yoyote inayohusika na ugomboaji kama itakavyoainishwa na mamlaka husika;

"maelekezo maalum" maana yake ni maelekezo ya mteja kwa Shirika kutekeleza hatua fulani wakati wa utoaji wa huduma;

"kuweka mzigo kwenye kontena" maana yake ni mchakato wa kupakia mzigo kwenye kontena na kufunga kontena kwa ajili ya kusafirishwa na usafirishaji wa baharini au wasafirishaji wa maji ya ndani;

Sura ya 148

"ankara ya kodi" ina maana sawa kama ilivyoelezwa chini ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani; na

"mtu wa tatu" maana yake ni mkandarasi, mkandarasi mdogo, msimamizi wa mkataba wa forodha, wakala au wafanyakazi wao waliopewa kazi na Shirika kufanya majukumu yake kwa niaba yake kama ilivyoainishwa kwenye Sheria na kanuni ya 4.

SEHEMU YA PILI
UTOAJI WA HUDUMA ZA KIPEKEE ZA UGOMBOAJI NA UONDOSHAJI

Huduma za kipekee za ugomboaji na uondoshaji

4.-(1) Shirika litatoa huduma za kipekee za ugomboaji na uondoshaji wa bidhaa za kipekee zifuatazo zinazoingizwa ndani ya nchi au kusafirishwa nje ya nchi:

(a) silaha na risasi;
(b) makinikia ya madini;
(c) kemikali zinazotumiwa na kampuni za madini;
(d) nyara za Serikali; na

Sura ya 283

(e) wanyama hai chini ya Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori.

(2) Mteja atahakikisha kuwa, bidhaa hazichanganywi na bidhaa za kipekee zilizopo chini ya mamlaka ya Shirika, katika nyaraka moja ya shehena.

(3) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (2), endapo nyaraka moja ya shehena imechanganya mizigo mingine iliyo chini ya mamlaka ya kipekee ya Shirika, Shirika

litagomboa shehena yote.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (3), Shirika litatoza ada, tozo au kamisheni ya ugomboaji.

Huduma zitakazotolewa na Shirika

5.-(1) Shirika litatoa huduma zifuatazo wakati linatekeleza majukumu ya kipekee chini ya kanuni ya 4:

(a) ugomboaji wa forodha;
(b) uwakala wa usafirishaji wa mizigo;
(c) ushauri wa kiforodha na usafirishaji wa mizigo; na
(d) huduma nyingine zozote kama zitakavyokubaliwa kati ya Shirika na mteja kwa kila shehena.

(2) Katika kutoa huduma zilizotajwa katika kanuni ndogo ya (1), Shirika litazingatia viwango vya utendaji vilivyowekwa.

(3) Endapo mteja anahitaji huduma iliyopo chini ya mamlaka ya kipekee ya Shirika kama ilivyoainishwa katika Sheria, kutakuwa na ombi kwa Shirika kutekeleza huduma za ugomboaji na uondoshaji wa shehena.

Kutekeleza kazi ya wakala binafsi wa meli

6.-(1) Endapo wakala binafsi wa meli anashindwa kutekeleza kazi zake, Shirika litahakikisha kazi hiyo inatekelezwa na kumtaka-

(a) wakala binafsi wa meli, ndani ya siku tatu, kukabidhi nyaraka zote muhimu za usafirishaji na taarifa kwa Shirika ili kuwezesha huduma hiyo kutolewa kama ilivyokusudiwa; na
(b) msimamizi mkuu wa meli kulipa ada zote za huduma ya uwakala wa meli zitakazofanyika.

(2) Shirika litaamua na kugawa hisa yoyote ya ada hiyo ya wakala binafsi wa meli ambaye leseni yake imesitishwa au kufutwa kwa huduma yoyote ambayo inaweza kuwa ilitolewa kabla ya kusitishwa au kufutwa kwa leseni yake.

SEHEMU YA TATU
MAKUBALIANO NA MTU WA TATU

Kutekeleza

7.-(1) Shirika linaweza kuingia mkataba na mtu wa

majukumu ya Shirika

tatu, pale litakapoona inafaa, kwa ajili ya kutoa huduma ya-

(a) uondoshaji kwa bidhaa za kipekee; na
(b) uwakala wa meli iwapo wakala binafsi wa meli ameshindwa kutekeleza majukumu yake.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), makubaliano yanaweza kuingiwa kupitia mkataba, makubaliano, ubia, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi au njia nyingine zinazoonekana zinafaa kwa Shirika.

Kushirikishwa kwa mtu wa tatu aliye na leseni au aliyesajiliwa

8. Shirika halitapanga, halitakasimu au halitashirikisha mtu wa tatu kutoa huduma zozote kwa niaba yake, isipokuwa kama mtu wa tatu ana leseni au amesajiliwa na mamlaka au taasisi husika kutoa huduma hiyo.

Upatikanaji wa mtu wa tatu
Sura ya 410

9. Shirika linaposhirikisha mtu wa tatu kufanya kazi zake, litafuata Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Masharti ya utoaji wa huduma

10.-(1) Mtu wa tatu atafuata vigezo na masharti ya makubaliano ya kutoa huduma yaliyoingiwa na Shirika.

(2) Wakati wa utekelezaji wa kazi za mkataba na Shirika, mtu wa tatu-

(a) atafanya kazi kwa uangalifu, weledi na uadilifu;
(b) atazingatia viwango vya utendaji vilivyoainishwa na Shirika; na
(c) atatekeleza majukumu kwa uaminifu.

Kamisheni inayolipwa kwa mtu wa tatu

11.-(1) Shirika litalipa kamisheni au malipo mengine kwa mtu wa tatu aliyeshirikishwa kutoa huduma ya uondoshaji mzigo, ndani ya siku saba baada ya kila mwisho wa mwezi wa kalenda.

(2) Kiasi kitakacholipwa katika kanuni ndogo ya (1) kitaainishwa katika makubaliano.

Uwajibikaji wa mtu wa tatu

12. Mtu wa tatu atawajibika kwa hasara yoyote, uharibifu au gharama itakayoingiwa na mtu yeyote kwasababu ya kushindwa, uzembe, uvunjaji wa sheria au kitendo kingine kisicho halali au kuacha kufanya jambo wakati wa kutekeleza kazi zake za huduma ya uwakala kwa niaba ya Shirika.

SEHEMU YA NNE
ADA, TOZO NA KAMISHENI

Ada, tozo na kamisheni zinazotumika

13. Ada, tozo au kamisheni zinazolipwa na wateja kwa Shirika kwa huduma inayotolewa chini ya Kanuni hizi zitapangwa na Bodi kama ilivyoainishwa katika Sheria na kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Akaunti ya amana ya mteja

14.-(1) Shirika litafungua akaunti ya amana ya mteja ya Shilingi za Tanzania, Dola za Marekani au sarafu nyingine yoyote kwa uhifadhi salama na usimamizi wa malipo ya awali ya mteja.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mteja anaweza kulipa kwenye akaunti ya amana ya wateja iliyofunguliwa ya Shirika, kiasi cha fedha kulipia gharama za huduma zinazotozwa kwa mteja, ikiwa ni pamoja na ada za uwakala, tozo, kamisheni na pesa inayorejeshwa.

(3) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (2), ada za uwakala, tozo, kamisheni, na pesa inayorejeshwa zitakatwa kutoka katika kiasi kilichowekwa amana, na Shirika litampa taarifa mteja baada ya kukamilika kwa miamala.

(4) Taarifa ya miamala ya mteja inayotolewa chini ya kanuni ndogo ya (3) itaonesha-

(a) kiasi kilichowekwa;
(b) kiasi kilichotumika;
(c) salio lolote la kurejeshewa fedha kwa mteja; au
(d) madai yoyote ya nyongeza ya Shirika.

Matumizi ya bakaa ya fedha ya mteja

15. Bakaa ya fedha iliyosalia katika akaunti ya amana ya mteja baada ya kukamilika kwa muamala inaweza kutumika kwa miamala ya siku zijazo au kurejeshwa baada ya maelekezo ya mteja kwa Shirika.

Njia na masharti ya malipo

16.-(1) Shirika, kupitia utoaji wa ankara ya kodi, litamjulisha mteja kulipa kiasi kikuu cha ada za uwakala, tozo au kamisheni pamoja na kodi inayotumika kwa huduma zitakazotolewa.

(2) Mteja atafanya malipo ambayo yameainishwa katika ankara ya kodi moja kwa moja kwenye akaunti ya makusanyo ya mapato ya Shirika kwa kutumia namba ya

udhibiti wa malipo iliyopatikana kutoka kwa Shirika

(3) Bila kujali ujumla wa kanuni ndogo ya (2), wateja wa mara moja na wateja wenye mizigo inayopita kupitia vituo vya mpaka watafanya malipo kama ilivyoainishwa katika ankara ya ushuru ndani ya masaa ishirini na manne kutoka tarehe ya ankara.

Kushindwa kufanya malipo

17. Kwa kuzingatia kanuni ya 16, endapo mteja ameshindwa kufanya malipo ndani ya muda ulioainishwa-

(a) Shirika halitaendelea kutoa huduma;
(b) kwa kuongezea katika jumla iliyoainishwa katika ankara ya kodi, mteja atatakiwa kulipa riba kwa kiwango cha asilimia kumi kitakachojumuishwa kila mwezi au sehemu ya malipo ya awali.

Malipo ya kamisheni

18.-(1) Mteja atawajibika kulipia ankara zote zinazohusiana na huduma zilizotolewa.

(2) Endapo Shirika litatumia fedha zake kulipa-

(a) kodi ya ongezeko la thamani baada ya mteja kuchelewa au kushindwa kulipia ankara ya kodi iliyotolewa ndani ya muda ulioainishwa; au
(b) malipo mengine yoyote yaliyotakiwa kulipwa na mteja,

Shirika litatoza kamisheni ya malipo kwa kiwango cha asilimia 2.5 kinachojumuishwa kila mwezi, au sehemu ya fedha zilizotumika.

Malipo ya sehemu ya utendaji

19.-(1) Endapo Shirika kwa kiasi fulani limefanya muamala ambao hauwezi kukamilika kutokana na kosa la mteja, Shirika litakuwa na haki ya kupokea malipo ya ada za uwakala na gharama iliyotumika kwa huduma iliyokamilika kabla ya kusitishwa kwa muamala huo.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), mteja atatakiwa kulipia gharama nyingine zinazohusiana, ikiwa ni pamoja na kodi na ushuru unaotumika kama inavyoweza kutakiwa na sheria nyingine.

(3) Kwa madhumuni ya kanuni hii, "kosa la mteja" litajumuisha yafuatayo:

(a) kushindwa kufanya malipo yanayohitajika;
(b) ufilisi au kufilisika kwa mteja;

(c) iwapo mali yoyote ya mteja inahusishwa katika tozo yoyote, kushikiliwa kwa mali, mgao wa jumla kwa manufaa ya wadai, maombi au mauzo kwa mdai au wakala wa Serikali;
(d) kufutiwa usajili, kusitishwa au kufutwa kwa leseni ya mteja;
(e) kushindwa kuwasilisha nyaraka yoyote inayohitajika na Shirika; au
(f) sababu nyingine yoyote itakayosababishwa na mteja ambayo inaweza kuzuia Shirika kutekeleza kazi zake chini ya Kanuni hizi.

SEHEMU YA TANO
VIGEZO NA MASHARTI YA BIASHARA

Utaratibu wa bima

20.-(1) Shirika linaweza, kwa maelekezo ya mteja, kuweka utaratibu wa bima wakati wa kutoa huduma chini ya Kanuni hizi isipokuwa iwapo-
(a) mteja amelipia bima na gharama za mchakato zinazoingiwa na Shirika kama inavyoweza kukubaliwa na mteja; na
(b) bima inategemea masharti na vigezo vya kawaida vya sera za mtoaji bima au mnufaika aliye hatarini.

Maelekezo ya mteja

21.-(1) Shirika litatoa huduma kwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na mteja.

(2) Maelekezo yanayotolewa na mteja chini ya kanuni ndogo ya (1) yatakuwa sahihi, kamili au kwa mujibu wa vigezo na masharti yaliyowekwa chini ya Kanuni hizi.

(3) Endapo mteja atatoa maelekezo yasiyo sahihi au kamili na yakasababisha hasara au uharibifu kwa Shirika au mtu wa tatu, Shirika litadai fidia ya hasara hiyo kutoka kwa mteja pamoja na gharama nyingine zozote zinazohusiana.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Shirika linaweza-
(a) kupanga utaratibu wa kutoa huduma na kuchagua; au
(b) kubadili utaratibu utakaofuatwa katika kushughulikia, kuhifadhi na kusafirisha shehena.

Uwasilishwaji wa shehena

22.-(1) Shirika litawasilisha shehena kwa mteja ndani ya muda uliowekwa kwa mujibu wa mpango wa ugomboaji shehena.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mteja anaweza, kwa kukosekana ushahidi unaothibitisha vinginevyo, kuchukulia kuwa, shehena limepotea na kuwasilisha madai ya fidia kwa Shirika baada ya siku mia moja na ishirini mfululizo kupita, baada ya tarehe iliyopaswa mzigo kufikishwa.

Upokeaji wa shehena

23.-(1) Mteja atathibitisha kupokea shehena kwa kusaini hati ya kupokea mzigo.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1) hati ya kupokea mzigo itakuwa ni ushahidi tosha kuwa shehena ilifikishwa katika hali nzuri na salama.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) na (2), iwapo mteja hajasaini hati ya kupokelea mzigo lakini amelipatia Shirika notisi ya maandishi wakati wa uwasilishwaji, ikibainisha hali ya jumla ya hasara au uharibifu wa shehena, itakuwa ushahidi tosha kuwa shehena hiyo haikufikishwa katika hali nzuri na salama.

Dhamana ya shehena

24. Shirika linaweza kushikilia shehena ya mteja na mali au nyaraka yoyote inayohusiana, kama dhamana ya kiasi chochote kinachostahili kulipwa kwa Shirika na kutumia dhamana hiyo kwa mujibu wa sheria.

Uthibitisho wa taarifa sahihi

25.-(1) Mteja atawasilisha kwa Shirika nyaraka zote zinazohusiana na shehena, na nyaraka hizo zitachukuliwa kuwa zinajumuisha taarifa sahihi kuhusiana na shehena, ikijumuisha maelezo asili ya jumla ya shehena, maelezo ya mzigo, alama na idadi, uzito, kiasi na wingi na uhatari wa shehena, kama yalivyotolewa na yeye binafsi au kwa niaba yake.

(2) Endapo mteja atashindwa kutoa taarifa sahihi chini ya kanuni ndogo ya (1), Shirika halitawajibika kwa kosa lolote, hasara au uharibifu unaohusiana na shehena hiyo.

Fidia

26.-(1) Shirika litawajibika kwa kiwango na kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), mteja atafidia Shirika kwa jukumu lolote lililofanywa wakati wa utekelezaji wa utoaji wa huduma za ugomboaji na uondoshaji kwa niaba ya mteja.

Wastani wa jumla

27. Shirika litalipwa fidia kuhusiana na madai yoyote ya wastani wa jumla ambayo yanaweza kufanywa kwa mteja, na mteja atatoa dhamana kama itakavyohitajika na Shirika.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA JUMLA

Ukomo wa madai ya hasara au uharibifu

28. Shirika halitawajibika kwa hasara au uharibifu wowote unaotokana na ukomo au hitilafu yoyote iliyo nje ya uwezo wa Shirika.

Wajibu wa Shirika

29. Shirika litatekeleza wajibu wa uangalizi ikiwa ni pamoja na kufanya uangalizi wa kina na hatua zinazofaa, kuhakikisha usalama na ulinzi wa shehena.

Tathmini ya fidia

30.-(1) Shirika, ndani ya muda unaofaa, litamfidia mteja kwa hasara au uharibifu wa shehena au upotevu wa fedha unaotokana na ukiukaji wa wajibu wa uangalizi.

(2) Endapo Shirika linatakiwa kulipa fidia kuhusiana na sehemu ya au shehena yoyote, tathmini itaamuliwa kwa kurejea thamani ya kawaida ya shehena ya aina na ubora unaofanana au njia nyingine yoyote kama Shirika litakavyoona inafaa.

Ukomo wa fidia

31.-(1) Shirika halitawajibika kwa hasara yoyote au uharibifu wa shehena, kwa kiasi kinachozidi Dola za Marekani elfu mbili au sawa na Shilingi za Tanzania kwa shehena iliyopotea au kuharibika, isipokuwa kama kiasi kikubwa zaidi kimerejeshwa na mtu ambaye Shirika linawajibika kwake.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), uwajibikaji wa Shirika kwa aina yoyote ya hasara ambayo haijatajwa chini ya Kanuni hizi, hautazidi jumla ya kiasi cha Dola za Marekani elfu tatu au kwa kiasi sawa na Shilingi za Tanzania kwa kila tukio isipokuwa kama kiasi

kikubwa kimepokelewa kutoka kwa mtu ambaye Shirika linawajibika kwake.

Ukomo wa uwajibikaji kwa kuchelewaji

32.-(1) Shirika litawajibika kwa malipo yanayotokana na uchelewaji katika kutoa huduma iwapo itathibitika kuwa, uchelewaji huo ulisababishwa na Shirika pekee.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), iwapo imethibitika kuwa, Shirika linawajibika kulipa tozo za uchelewaji katika kutoa huduma, kuwajibika huko kutakuwa kwa kiasi kisichozidi gharama zinazohusiana na huduma iliyosababisha ucheleweshaji huo.

Jukumu la usiri

33.-(1) Mwajiriwa, wakala au mwakilishi wa Shirika hatatumia kwa maslahi binafsi wakati wowote au kwa namna yoyote moja kwa moja au vinginevyo, kufichua au kuwasiliana kwa njia yoyote, taarifa yoyote ambayo ni miliki ya mteja.

(2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), Shirika litatakiwa kulinda taarifa yoyote ya mteja na kuzichukulia kama za siri, isipokuwa inapohitajika kufichua taarifa hizo kwa mujibu wa sheria.

Uzingatiaji wa taratibu zilizoanzishwa za biashara

34. Katika kutekeleza shughuli zake, Shirika, pamoja na sheria na kanuni husika, litazingatia taratibu za kutoa huduma, zikijumuisha-

(a) kutoa huduma kwa saa ishirini na manne kila siku kwa siku saba za wiki ikijumuisha siku za mwisho wa juma na sikukuu za kitaifa;
(b) kuweka wazi ada, tozo na kamisheni zinalipwa na mteja;
(c) kuanzisha mfumo wa kushughulikia malalamiko;
(d) kukusanya nyaraka za kupokelea mzigo;
(e) kukusanya nyaraka za uhifadhi; na
(f) kumjulisha mteja kuhusu hatua za usafirshaji wa mizigo.

Utaratibu wa kushughulikia

35. Endapo mtu ana mgogoro wowote unaohusiana na jambo lolote linalotokana na-

(a) utekelezaji wa majukumu ya Shirika; au

malalamiko

(b) utekelezaji wa Sheria na Kanuni hizi,

TS. Na. 338 ya 2018

anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa mujibu wa Kanuni za Kushughulikia Malalamiko.

Kufuta TS. Na. 386 la 2020

36. Kanuni za Huduma ya Biashara ya Meli Tanzania za Mwaka 2020 zimefutwa.

Dodoma,
5 Machi, 2025

MAKAME M. MBARAWA
Waziri wa Uchukuzi